Wananchi Wa Lamu Ni Wafuasi Wa Nyao-Mzamil

MBUNGE wa Lamu Mashariki, Bw. Mzamil Omar Mzamil amewashukur wananchi wa sehemu hiyo kwa kumpa uwezo tena wa kuwawakilisha Bungeni kwa kipindi cha miaka mitano ijayo na akaahidi kuwatumikia akiwa kama mtumishi wao.
Ripoti Abdulrahman Sheriff.

Akitoa shukrani hizo kupitia kwa *COASTWEEK*, Bw. Mzamil aliwasifu watu anaowawakilisha kwa moyo waliouonyesha toka wakati wa kampeni hadi uchaguzi ulipofika na jinsi walivyoendesha mambo yao kwa amani kwa kuzingatia filosofia ya Nyayo.

Alisema Bw. Mzamil: "Wananchi wa Lamu Mashariki wamepevuka kisiana na ni watu ambao wana imani kamili na maongozi ya busara ya Mtukufu Rais Daniel arap Moi Tutaendelea kumuunga mkono Rais Moi katika kudumisha amani, umoja na upendo."

Mbunge huyo alishinda kiti cha Lamu Mashariki baada ya kuwabwaga wapinzani wake wawili, Mabwana Somo Abu Somo na Omar Saggaf.

TOFAUTI

Bw. Mzamil aliwaomba wananchi wa sehemu hiyo wasahau tafauti zao na washirikiane katika kazi za ujenzi wa taifa. "Hatuna budi kuanza mara moja shughuli za maendeleo na kuacha mambo yaliyopita ya uchaguzi", akasema Mbunge huyo.

Naye Tamimu wa Thalatha Twaifa, Sheikh Mohammed Salim Shirazy alimpongeza Rais Moi kwa kuchagua Baraza la Mawaziri ili kuanza kazi zao baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika mnamo Septemba 26, mwaka huu.

Sheikh Shirazy aliliambia *COASTWEEK* kwamba Rais Moi amewateua Mawaziri na wakuu wengine akiwa na imani watatumika kwa uaminifu wa kulileta taifa hili ufanisi na ni juu ya wale waliopewa madarak hayo watumike ipsavyo.

RAIS

Alisema: "Rais hakuchaguwa Baraza lake la Mawarizi kwa ajili ya ukabila, dini ama rangi bali amewapa hatamu za uongozi akiwa na uhakika watatumikia wananchi na kuleta matunda ambayo yatawanufaisha wakenya wote".

Sheikh Shirazy pia alimtumia pongezi Bw. Hussein Maalim Mohammed kwa kuchaguliwa kuwa mmoja kati ya Mawaziri watatu ambao watatumika katika Afisi ya Rais na akawa na matumaini atafanikiwa kwenye kazi hiyo.

Bw. Hussein Maalim Mohammed aliyenyakua kiti cha Garissa Kati wakati wa uchaguzi uliopita, ni Mwislamu wa kwanza nchini kupewa madaraka ya Uwaziri. Pia ni mbunge wa kwanza kutoka Mkoa wa Kaskazini Mashariki kuwa na cheo cha Uwaziri toka Kenya iwe huru.

WAKAZI Wa Wundanyi na sehemu zingine za Taita wamefurahishwa sana na kuchaguliwa kwa Bw. Mwashengo Mwachofi kuwa Mbunge tena.

Ningependa kwamba wananchi wa sehemu hii wawe na mtindo huo huo wa kuchagua viongozi bora kwa shabaha ya maendeleo.

Nawaomba ambao walioshindwa katika uchaguzi waungane na Mwachofi kusukuma gurudumu la maendelo wilayani.

Na pia nashukuru madiwani waliochaguliwa na kuwasihi waondoe tofauti zao na kushirikiana ili kuleta maendeleo ya haraka.

Mnyika Mwaigho,
Magongo, MOMBSA.

MKUU Msimamizi wa B.A.T. Pwani Bw. William Juma akiamkuana na Bw. Nassir katika Shamra Shamra za Sherehe za Kenyatta Dei Kwenye ukumbi wa Oceanic Hotel Mombasa.
PICHA: CEASAR MADDANGANHA.

Muses Atunukiwa

VITABU viwili, kimoja cha Kiengereza *"NYAYO ERA AND CULTURE"* na kingine cha Kiswahili *"Insha za Busara"* vimetunukiwa Mohamed Naaman Muses kwa urafiki wake mwema na mtungaji wa vitabu hivyo, Faraj Dumila.

Mohamed Naaman Muses ameelezwa kama rafiki wa chanda na pete na watokea utotoni mwao amekuwa akimsaidia rafikiye Faraj Dumila kwa hali na mali katika shughuli zake za kibanfsi na za kiutamaduni wa nchini Kenya.

• BW. MUSES

TUNU

Vitabu hivyo ni tunu ya aina ya pekee kwa Bw. Muses, na kielelezo cha shukrani halisi zitokazo kwa mwadishi huyu mashuhuri nchini Kenya na hata bara zima la Afrika kwani vitabu vyake sasa vitakwenda huko Nigeria na Zambia na hata Misri kwani vimetambuliwa kama msingi wa uendeshaji na ukuzaji wa Utamaduni wa Kenya na vile vioo vyake vinavyo mulika mila na nyendo za wafanyikazi wa magazetini.

• FARAJ DUMILA

Kitabu chake cha Kiengereza, sehemu ya pila kimapata ujumbe maalumu kutoka kwa mwandishi mashuhuri na mwana siasa shupavu Dr. Taaitta Toweett, ambaye ni Mbunge Maalum na Mwenyekiti wa shirika la 'Kenya Airways'. Katika risala ya Dr. Doweett amemsifu Faraj Dumila kwa juhudi zake za kueneza shughuli za kitamuduni nchini Kenya na kusambaza mithali za Hekima za Mwazilishi wa Taifa la Kenya, Mzee Jomo Kenyatta na Johari za Hekima za Mtukufu Rais Moi.

Vitabu hivi ni mionongoni mwa harakati za kusherehekea Mwaka wa Ishirini Tokea Kenya Ijipatie Uhruru wake. Sehemu ya tatu ya "Nyayo Era And Culture" iko njiani hapo mnamo 12/12/83 wakati wa siku kuu ya jamhuri.

Kisura wa Taita

Tishio la mji ni Binti Joyce Mwazuna mwenye umri wa miaka 21 na mzaliwa halisi wa Wundanyi Wilayani Taita/Taveta. Kwa sasa anachapa kazi barabara katika Shirika la Tumbaku (BAT) Mombasa. Anapendelea sinema, magoma na kujistarehesha na Coastweek kila Ijumaa

PICHA: CEASAR MADDANGANHA.

Asemavyo Mhariri:

Wakenya Wangali Wafalme Wa Riadha

KENYA kwa mara nyingine, imefanikiwa kushikilia ufalme wa Wanariadha katika Afrika Mashariki na Kati wakati wanariadha wake walipohifadhi tena kombe kwenye mashindano yaliyofanyika uwanja wa Bugembe Stadium mjini Jinja nchini Uganda.

KWENYE Mashindano hayo ambayo yalishrikisha mataifa matano - Kenya, Uganda, Misri, Tanzania Bara na Zanzibar - Wanariadha wa Kenya walionyesha Ujasiri na upendo mkubwa kwa taifa lao na hawakukubali kuadhiriwa, hasa wakifahamu vile walivyofanya vibaya huko Helsinki nchini Finland.

NIKIWA nimeshuhudia kwa macho yangu vile Wakimbiaji wetu walivyokuwa na moyo mkubwa wa kuihami nchi yao, sina budi kuwa na imani watafanikiwa kutuletea kapu la Medali wakati wa Mashindano ya Olympic ambayo yatafanyika katika mji wa Los Angeles huko Marekani mnamo Julai na Agosti, mwakani.

MARA baada ya Waziri Mkuu wa Uganda, **Bw. Eric Otema Alimadi** kuyafungua Mashindano hayo, Wakenya walianza kuonyesha ujasiri wao katika uwanja wa Riadha kwa kunyakuwa medali kadha na hata mwisho wa michezo hiyo wakawa washindi; ushindi ambao haukuwa rahisi bali wa jasho na ambao pia ulipatikana kutokana na hima ya wanariadha wetu na maafisa wake.

INGAWA tuna furaha kwa wanaspoti kutuletea tena ubingwa katika Afrika Mashariki na Kati, ushindi huo hautokuwa na maana sana kama tutashindwa kufanya uzuri wakati wa michezo ya Olympic 1984. Kwani twataka tupokee medali nyingi kama vile wakenya wengine walivyokuwa wakituletea miaka ya nyuma.

MIPANGO yahitajika kufanyika mapema kuitayarisha timu yetu na kuwafanya Wanariadha wetu wawe na mioyo ya kuihami nchi yao kama vile miamba ya zamani akina **Kipchoge Keino**, Naftali Temu, Ben Jipcho, Samason Kimombwa, **Henry Rono**, Amos Biwott, Robert Quko, Charles Asati, Julius Sang na Hezekiah Nyamau na wengineo ambao walijitolea kidhati kuletea siga Kenya.

UMEFIKA wakati ambapo maafisa ambao wanahusika na Riadha hasa wa Kenya Amateur Athletics Assoication, Baraza la Michezo la Kenya National Sports Council na Baraza la Michezo ya Olympiki yaani Olympic Sports Council wafanye tartibu za kuharakisha maandalizi ya timu itakayotuwakilisha.

LAZIMA maafisa wa vyama hivyo ambavyo nimevitaja hapo juu watayarishe mipango mizuri kwa Wanariadha wetu ili nao wawe na mioyo ya kuweza kuwafurahisha Wakenya kwa kushinda mbio na kuweza kutukumbusha wakati ambapo Wakenya walikuwa wakijulikana kwa uhodari wa kutimua mbio kama Swara! -

Abdulrahman Sheriff
—NJINJA (Uganda)

Farucci Coastweek

JISHINDIE VIATU MARIDADI
VYA FARUCCI KWA MSHINDI
WA KWANZA NA T-SHIRT
KWA WASHINDI WA PILI
NA WATATU KATIKA SHINDANO
JIPYA LA KUJAZA MANENO

SWAHILI CROSSWORD No. 173



KWENDA KULIA:

1. Sumu ya nyoka au ya mshale.
5. Silaha ya kuwindia ndege.
6. Tenzwa nguvu.
7. Moja katika makontinenti ya dunia.
9. Jina la kibaniani
12. Ndani kwa kimombo.
13. majani ya mnazi
14. Medical Officer
15. Sana
16. Chombo kama bangili.
17. Namna ya kukaa
18. Jitu zima.

KWEND CHINI:

1. Mti unaosaidia chombo kukipeleka maji mengi.
2. Kiungo cha mchuzi.
3. Sehemu ya juu ya kichwa.
4. Duara, Mvingo, ua.
8. Kinyume cha iuze
10. Aina ya mti.
11. Sikiza mwito.
14. Karne moja.
16. Ufupi wa "kazana kusoma".

Wshindi wa Fumbo La Kujaza maneno No. 172.

1. S. A. Msaada, Sanduku La Posta 98106, MOMBASA.
2. Islam Ali Swedan, Sanduku La Posta 62, MARIAKANI.
3. Miss Madango Essau, Sanduku La Posta 85390, MOMBASA.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANANO No. 172.

KWENA KULIA

1. BAWABU, 5. JUA, 6. RAFIKI, 8. MA, 10. KIRIBA, 12. KAMATANA, 15. UN, 16. MKIZI, 18. AKUTOE, 19. SI.

KWENDA CHINI

1. BARAKA, 2. ALIKA, 3. UJIRA, 4. KAMBA, 7. KITAMBO, 9. AA, 11. INDIA, 13. MUNYU, 14, BISI, 17. UA.

JINA. ....

SANDUKU LA POSTA. ....

....

Shindano la Fumbo La kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata viatu na T-Shirt maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* limited Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwe Muhariri *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatano tarehe **Nov. 9, 1983**, saa nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.